

## **Isemavyo Biblia.....**

### **Kuhusiana na Ubatizo**

#### **Na Willy Emmanuel**

“Na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti kwa kufunua uzima na kutokuharibika kwa ile injili,” 2 Timotheo 1:10

Kwa kuwa Yesu alimnyang’anya shetani funguo za dhambi na mauti (Ufunuo 1:18), sasa mtu anaweza kupatanishwa kwa Mungu na kuokoka kwa njia ya mauti na uzima wa Yesu (Warumi 5:10). Upatanisho na wokovu upo kwa wale watii.

Katika Warumi 6:3-6,17-18 twaweza kusoma habari ya ujumbe wa injili unaotufundisha jinsi ya kuupokea wokovu. Hapa Biblia inatufundisha ya kwamba ubatizo ni kuzikwa pamoja na Kristo kwa kuusulubisha utu wetu wa kale ule wa dhambi pamoja naye na ndiposa unapobatizwa unainuka ukiwa kiumbe kipya katika Kristo. Hii ni habari njema isiyo kifani! Tuwapo dhambini, dhambi ambazo hutufarakanisha na Mungu, sasa dhambi hizo zinaweza kuoshwa (Matendo 22:16) tunapokutana kwa njia ya ubatizo katika damu iliyo ya thamani mno ya mwokozi wetu (Ufunuo 1:5)

Ingawaje leo kuna mafundisho mengi kuhusiana na ubatizo, lipo fundisho moja tu ambalo ndilo la kweli na limetoka kwa Mungu. Nalo ni lile lisemalo “Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa, Marko 16:16. Katika Yohana 3:5 “Yesu akajibu, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.” Katika matendo 2:38, mnamo siku ya pentekoste ya kwanza baada ya kupaa kwa Bwana Yesu, Petro kwa njia ya Roho mtakatifu akasema, “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu,”

Imeandikwa “mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowakoa ninyi pia siku hizi,” 1 Petro 3:21. Tafadhali uwe huru kutupigia simu endapo una swali lolote lihusulo ukweli kuhusu ubatizo.